**Tangazo la Serikali Na. 373 la Tarehe 03/10/2014**

**SHERIA ZA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)**

**(SURA YA 287)**

**SHERIA NDOGO**

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 88(1))*

## HATI RASMI (UANZISHAJI WA BODI YA MFUKO WA PEMBEJEO ZA KILIMO) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO, ZA MWAKA 2014

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

**1.** Hati rasmi hii itajulikana Kama Hati Rasmi (Uanzishaji wa Bodi ya Mfuko wa Pembejeo za Kilimo) za Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

**2.** Hati rasmi hii itatumika katika eneo lote lililoko chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo.

Tafsiri

**3.** Katika Hati rasmi hii isipokuwa kama itatamkwa vinginevyo;

"Afisa Kilimo wa Halmashauri" maana yake ni Mtumishi wa Umma ambaye ndiye Msimamizi Mkuu wa utoaji wa huduma za Kilimo katika Halmashauri.

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Mfuko wa Pembejeo za Kilimo ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo iliyoanzishwa chini ya Kifungu cha 4(1) cha Hati rasmi hii.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Rombo.

"Kamati ya Uchumi na Mazingira ya Halmashauri" Maana yake ni Kamati ambayo imeanzishwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya)

"Kamati ya Utendaji ya Mfuko wa Pembejeo" maana yake ni Kamati iliyoteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Hati rasmi hii.

"Katibu Mtendaji" maana yake ni Mtendaji Mkuu wa Mfuko wa Pembejeo wa Halmashauri aliyajiriwa na Bodi ya Mfuko wa Pembejeo kwa mujibu wa Kifujgu cha 21 cha Hati rasmi hii.

"Mfuko wa Pembejeo" maana yake ni mfuko wa Pembejeo ulioanzishwa kwenye Halmashauri kwa mujibu wa Hati rasmi hii.

"Mkuu wa Wilaya" maana yake ni Mkuu wa Wilaya ya Rombo.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Timu ya Uendeshaji ya Mfuko" maana yake ni Timu ya Wataalamu inayoshughulikia shughuli za kila siku za Mfuko.

"Pembejeo za Kilimo" maana yake ni zana inayomsaidia Mkulima katika kilimo kama mbegu, trekta, madawa n.k.

Bodi.

**4.** -(1) Kutakuwa na Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Mfuko wa

Pembejeo za Kilimo ambayo itawajibika kwa Halmashauri.

(2) Bodi itaundwa na Wajumbe wafuatao-

(i) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti watakaochaguliwa miongoni mwa wajumbe wa Bodi na watashika madaraka kwa kipindi cha miaka mitano na wawe na uzoefu na masuala ya Kilimo.

(ii) Wawakilishi Watano kutoka katika Tarafa za Halmashauri.

(iii) Mwakilishi mmoja kutoka miongoni mwa Madiwani wa Halmashauri.

(iv) Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira wa Baraza la Halmashauri.

(v) Katibu wa Bodi ataajiriwa na Bodi ya Mfuko na ndiye atakuwa Katibu wa Mikutano yote ya Bodi.

Kipindi cha kushika madrasa

**5.** Wajumbe wa Bodi watashika madaraka kwa kipindi cha Miaka Mitano, lakini Mjumbe anaweza kuteuliwa tena na kuendelea kuwa madarakani kwa kipindi kingine cha Miaka mitatu.

Ofisi za Bodi

**6.** Ofisi za Bodi zitakuwa katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri.

Utaratibu wa kujaza nafasi wazi.

**7.** -(1) Pale ambapo nafasi katika Bodi zitakuwa wazi aidha kwa kifo, kujiuzulu, ugonjwa, au kwa sababu nyingine yeyote ile.Mjumbe mwingine atateuliwa kujaza nafasi hiyo kwa kipindi kilichobaki.

(2) Hakuna uchaguzi utakaofanywa endapo kipindi kilichobaki ni chini ya miezi sita.

(3) Mjumbe atakayeteuliwa kutokana na Sheria Ndogo ya 9(1) hapo juu ataweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

Uteuzi Bodi kuthibitishwa na Baraza la Madiwani

**8.** **-**(1) Uteuzi wa wajumbe utathibitishwa na baraza la madiwani la Halmashauri.

Uzinduzi wa Bodi

(2) Bodi itazinduliwa rasmi kwa kushuhudiwa na Mkuu wa Wilaya baada ya kuithibishwa na Baraza la Madiwani.

Bodi kuvunjwa kwa kuzembea kazi

**9.** **-**(1) Endapo Bodi itazembea kazi au itashindwa kutekeleza kazi zake, Halmashauri itaionya Bodi mara mbili kwa maandishi au kuvunja Bodi na kuandaa uteuzi mpya ndani ya miezi miwili

(2) Endapo Bodi itavunjwa, wajumbe wote wa kuteuliwa watapoteza nafasi zao na hawatateuliwa tena kuwa wajumbe wa Bodi ya Mfuko wa Pembejeo za Kilimo

(3)Wakati Bodi imevunjwa. Kamati Tendaji ya Mfuko wa Pembejeo itatekeleza majukumu ya Bodi hadi hapo Bodi mpya itakapochaguliwa.

Vikao vya Bodi

**10.** **-**(1) Bodi itafanya Vikao vyake vya Kawaida kila baada ya miezi mitatu na Vikao vyote vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti. Endapo Mwenyekiti hatakuwepo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao kama wote hawatakuwepo kwa pamoja, Mjumbe mmoja atachaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe kuwa Mwenyekiti wa Kikao na kura za

kumchagua zitatakiwa ziwe nusu ya Wajumbe wote wa Kikao.

(2) Vikao vya dharura vitafanywa pale tu Mwenyekiti atakapoomba au kuombwa kufanya hivyo kwa maandishi na kupata idhini ya Wajumbe wasiopungua nusu ya Wajumbe wote wanaopiga kura.

(3) Mjumbe yeyote ambaye bila taarifa au sababu ya msingi atashindwa kuhudhuria vikao mfulilizo vya Bodi atakuwa amepoteza sifa za kuendelea kuwa Mjumbe wa Bodi na nafasi yake itatangazwa kuwa wazi.

Bodi kualika Wadau kwenye vikao

**11.** Bodi inaweza kualika watu wengine kwenye vikao vyake kama kutakuwa na haja ya kufanya hivyo lakini hawatakuwa na haki ya kupiga kura.

Kumbukumbu za mikutano ya Bodi.

**12.** Bodi itahakikisha kumbukumbu za Mikutano yake yote zinaandikwa na kuhifadhiwa, pia kumbukumbu za kila Mkutano zitathibitishwa na Bodi kwenye mkutano unaofuata na zitatiwa saini na Mwenyekiti wa Mkutano pamoja na Katibu.

Ada ya vikao na uwezo wa kuamua

**13.** -(1) Nusu ya Wajumbe wote ndiyo itakuwa akidi kamili katika Vikao vyote vya Bodi.

(2) Uamuzi wa Bodi utakuwa ni ule unaoungwa mkono na Wajumbe zaidi ya nusu ya Wajumbe kamili wa Bodi.

(3) Wajumbe wa kuchaguliwa wa Bodi ndio watakaokuwa na uwezo wa kupiga kura na kupitisha uamuzi wa Bodi

(4) Wataalamu na waalikwa hawatakuwa na haki ya kupiga kura.

(5) Kila Mjumbe wa Bodi atakuwa na kura moja na iwapo itatokea kura kufungana, Mwenyekiti wa Bodi atakuwa na kura ya ziada mbali na kura yake ya kawaida.

Sifa za kuwa mjumbe wa bodi.

**14.** -(1) Mtu anaweza kushika nafasi ya ujumbe wa Bodi kama atakuwa na sifa zifuatazo-

(a) Awe raia wa Tanzania

(b) Awe na umri usiopungua miaka kumi na nane

(c) Awe na akili timamu.

(d) Awe na uelewa juu ya kilimo.

(e) Asiwe na madaraka yoyote kwenye chama cha Siasa.

(2) Mfanyakazi wa Halmashauri hataruhusiwa kuwa Mjumbe wa Bodi.

Majukumu na kazi za Bodi.

**15.** Majukumu na kazi za Bodi zitakuwa kama ifuatavyo-

(a) Kubuni Mipango na Mikakati kwa ajili ya maendeleo ya Kilimo katika Halmashauri.

(b) Kusimamia utekelezaji wa manunuzi na mgawanyo wa pembejeo za kilimo kwa Wakulima kwa mujibu wa Msimu wa kilimo Wilayani.

(c) Kupitia mpango wa maendeleo ulioandaliwa na Mhasibu na kuuthibitisha kwenye bajeti ya mwaka na kuangalia vyanzo na

bei za pembejeo zinaendana na mahitaji ya Wilaya.

(d) Kutekeleza maazimio na maelekezo yote ya Mkutano Mkuu wa Mwaka.

(e) Kuteua Mkaguzi wa Mahesabu wa kukagua mahesabu na vitabu vya mahesabu ya kila mwaka.

(f) Kuteua watia saini Akaunti za Mfuko wa Pembejeo

(g) Kuhakikisha Akaunti za Mfuko zipo wazi.

(h) Kuandaa taarifa ya mahesabu ya mwaka katika Mkutano Mkuu wa Mwaka baada ya ufungaji wa vitabu vya mwaka.

(i) Kusimamia na kutekeleza maazimio na maelekezo ya Mkutano Mkuu wa mwaka wa Bodi.

(j) Kuteua msambazaji/mfanyabiashara mwaminifu kununua na kusambaza pembejeo za kilimo na kuzuia kwa wakulima kupitia Kamati za Maendeleo za Kata na Vyama vya Msingi ngazi Vijijini.

(k) Kukagua na kuhakikisha pembejeo za kilimo zinatolewa/zinazonunuliwa kwa kutumia fedha za mfuko zinakuwa katika hali ya ubora unaokubalika.

(l) Kuingia Mikataba na kuwa na ushirikiano na Taasisi mbali mbali, Serikali, Mawakala zinazojihusisha na Pembejeo za

Kilimo kwa manufaa ya wakulima wilayani.

(m) Kusimamia utekelezaji na kutathmini Mipango ya Kilimo katika Halmashauri.

(n) Kujadili na kurekebisha Mipango na Bajeti ya Kilimo na kuiwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa mwaka wa Utendji kwa ajili ya kuidhinishwa;

(o) Kupokea, kuchambua na kuidhinisha Taarifa za Utekelezaji wa Mfuko wa Pembejeo wa Halmashauri.

(p) Kubuni vyanzo mbali mbali vya mapato na rasilimali za kutosha kuendesha Mfuko wa Pembejeo wa Halmashauri.

(q) Kushirikiana na Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira ya Halmashauri;

(r) Kuratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya Kilimo katika Halmashauri kulingana na program za kitaifa.

(s) Kupitisha Kanuni za Utengaji na Utumiaji wa Fedha kutoka kwenye Mfuko kwa ajili ya kuendneleza Mfuko.

(t) Kusimamia mapato na matumizi ya Mfuko katika Halmashauri.

(u) Kufanya jambo lolote litakalofanikisha maendeleo ya Kilimo katika Halmashauri.

Mamlaka ya Bodi.

**16.** Bodi itakuwa na Mamlaka yafuatayo-

(a) Kusimamia mgawanyo wa fedha zinazoingizwa kwenye Mfuko wa Pembejeo za Kilimo wa Halmashauri.

(b) Kuajiri Mhasibu na Katibu Mtendaji ambaye atakuwa katibu wa Bodi na kuachisha kazi watumishi wa Bodi.

Maagizo na maekelezo

**17.** Maagizo, maelekezo, taarifa au hati nyingine zilizotengenezwa au kutolewa kwa niaba ya Bodi zitatiwa saini na-

(a) Mwenyekiti wa Bodi au

(b) Katibu Mtendaji au Afisa mwingine yeyote aliyeidhinishwa kwa maandishi na Katibu Mtendaji wa Bodi kwa ajili hiyo.

Uhusiano wa Bodi na wadau na mamlaka nyingine.

**18.**-(1)Uhusiano wa Bodi na Jamii, Wadau na Mamlaka nyingine utakuwa kama ifuatavyo-

(a) Bodi itahakikishaWakulima wanashirikishwa kikamilifu katika kutambua matatizo, kuweka kipaumbele, kupanga, kuchangia, kufuatilia na kutathmini hali ya kilimo;

(b) Bodi itawajibika mbele ya Halmashauri ambapo mipango ya kilimo ya Robo mwaka pamoaja na taarifa za kitaalam za fedha zinapitiwa na kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira na Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango na baadaye kuthibitishwa na Baraza la Halmashauri.

(c) Bodi itaendesha shughuli zake kwa utaratibu wa uwazi na ambao utakuwa na ufanisi kwa Halmashauri na vyombo vyake vingine

vya utendaji bila ya Halmashauri kuingilia uhuru wa Bodi.

(2) Bila ya kuathiri maelekezo yaliyomo katika Sheria Ndogo ya (1) ya Hati rasmi hii Bodi inaweza kukasimu baadhi ya madaraka yake pale inapoona inafaa.

Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira ya Halmashauri.

**19.** Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira ya Halmashauri itafanya kazi zifuatazo-

(a) Itapokea Mipango yote ya Maendeleo ya Mfuko

(b) Itapokea taarifa za Ukaguzi wa Hesabu za Mfuko na kupitia hoja za Ukaguzi na baadaye kuziwasilisha kwenye Halmashauri ambayo itajadili na kuiwasilisha kwa Mkuu wa Wilaya.

Jukumu la Wizara.

**20.** Jukumu la Wizara za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Kilimo, Ushirika na Mifugo zitakuwa ni kuandaa Sera, kupanga viwango, kufuatilia na kusimamia shughuli za Bodi kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Katibu Mtendaji.

**21.** Bodi kwa idhini ya Mkutano Mkuu wa Mwaka, itamteua Katibu Mtendaji wa Mfuko wa Pembejeo za Kilimo wa Halmashauri.

Uteuzi wa katibu Mtendaji

**22.**-(1)Nafasi ya katibu Mtendaji itatangazwa katika magazeti yanayosomwa zaidi nchini na Bodi itamteua mtu ambaye atakabidhi vigezo vya uteuzi na ambaye atakuwa na sifa zinazofaa.

(2)Bodi itaamua sifa za watu ambao wataomba nafasi ya katibu Mtendaji.

(3) Katibu Mtendaji atakuwa na muda maalum wa kushika madaraka kama itakavyopangwa na Bodi.Isipokuwa tu kwamba kipindi kimoja cha

madaraka kisizisi miaka mitano na mtu aliyeko madarakani anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

Kazi za katibu Mtendaji

**23.** Kazi za Katibu Mtendaji wa Bodi zitakuwa-

(a) Kuwa Mtendaji Mkuu wa Shughuli zote za Mifuko na Katibu wa Vikao vyote vya Bodi atasaini mihtasari na maazimio yote yaliyofikiwa kwenye mikutano.

(b) Kuandaa agenda za Vikao kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Bodi.

(c) Kuweka kumbukumbu za Vikao na Taarifa mbalimbali za Bodi sehemu salama.

(d) Kuongoza, kupanga na kuratibu utendaji wa shughuli za kila siku za Mfuko.

(e) Kubuni, kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mipango ya maendeleo ya Mfuko.

(f) Kubuni na kushauri vyanzo mbali mbali vya mapato vya Mmfuko wa Pembejeo wa Halmashauri.

(g) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Pembejeo wa Halmashauri.

(h) Kubuni na kushauri mbinu mbalimbali za kukuza na kuendeleza Mfuko wa Pembejeo wa Halmashauri.

Vyanzo vya mapato.

**24.** Vyanzo vya mapato vya Mfuko wa Pembejeo vitakuwa kama ifuatavyo-

(a) Makato yanatokana na mauzo ya kahawa kutoka kwa wafaidika wa Mfuko (Wakulima na Wafanyabiashara wa

mazao).

(b) Faida inayotokana na mauzo ya Pembejeo za kilimo kama mbolea.

(c) Ruzuku mbali mbali

(d) Misaada mbalimbali kutoka Serikalini, Nchini mbalimbali, taasisi za kimataifa na kitaifa, Mashirika ya Watu binafsi na kiserikali, Makampuni binafsi, na madhehebu ya Dini.

(e) Mchango kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Rombo.

(f) Mikopo ;na

(g) Vyanzo vingine halali vya mapato.

Fedha za Mifuko kulipwa kwenye Akaunti.

**25.** Fedha zote zitakazokusanywa kama fedha za Pembejeo zitalipwa kwenye akaunti za Benki kama Bodi itakavyoona inafaa au kuagiza.

Akaunti maalum ya Mfuko wa Elimu

**26.-**(1)Kutakuwa na Akaunti Maalum ya Mfuko wa pembejeo wa Halmashauri ambao fedha zote zitawekwa na kutunzwa.

(2) Bodi itaajiri Mweka Hazina atakayesimamia Akaunti za zitatumika kwa madhumuni ya kuendeleza, kukuza na kuboredha Kilimo

(3) Bodi itaajiri Mweka Hazina atakayesimamia Akaunti za Mfuko wa Pembejeo na kutunza mahesabu yote ya mapato na matumizi.

Matuamizi ya

**27.** Fedha zitakazowekwa kwenye Mfuko wa Pembejeo zitatumika kwa

Fedha.

madhumuni ya kuendeleza, kukuza na kuboresha Kilimo kama itakavyokuwa katika Mpango wa maendeleo ya Kilimo wa Halmashauri.

Bodi kuidhinisha malipo.

**28.** Bodi inaweza kuidhinisha malipo ya fedha kutoka kwenye mfuko kwa madhumuni ya kulipia gharama za;

(a) Ununuzi wa Pembejeo katika Halmashauri

(b) Uendeshaji wa Bodi

(c) Miradi na program zinazogharamiwa na Mfuko

(d) Udhamini wa Wakulima katika Pembejeo katika kukuza kilimo.

(e) Shughuli nyingine yoyote au zozote ambazo kwa maoni ya Bodi zina manufaa kulingana malengo na madhumuni ya Mfuko.

Kamati Tendaji.

**29.** -(1) Kutakuwa na Kamati ya Utendaji ya Mfuko wa Pembejeo wa Bodi.

(2) Kamati Tendaji itakuwa na Wajumbe wafuatao-

(a) Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ambaye atakuwa Mwenyekiti.

(b) Katibu Mtendaji wa Bodi ambaye atakuwa katibu.

(c) Afisa Kilimo wa Halmashauri ambao watakuwa Wajumbe.

(d) Mweka hazina wa Bodi ambaye atakuwa Mjumbe

(e) Afisa Mipango wa Halmashauri ambaye atakuwa Mjumbe

Kazi za Kamati

**30.** Kazi za Kamati Tendaji zitakuwa kama ifuatavyo-

(a) Kuandaa mipango kabambe ya Kilimo Kwanza ya Halmashauri ambayo itatilia mkazo mahitaji yote ya Kilimo ya Halmashauri kwa kuzingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Mpango wa Kilimo Kwanza;

(b) Kuwezesha na kuratibu Vikao vya Bodi ya Mfuko wa Pembejeo pamoja na Mkutano Mkuu wa mwaka.

(c) Kuchambua na kuhamisha maeneo ya kipaumbele kwa masuala ya Kilimo katika Halmashauri.

(d) Kuweka taratibu za vigezo vya usambazaji wa Pembejeo ya ruzuku kwa Wakulima katika Halmashauri.

(e) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa Mfuko wa Kilimo na maendeleo ya Kilimo katika Halmashauri.

Mkutano Mkuu wa mwaka.

**31.** Kutakuwa na mkutano Mkuu wa Mwaka wa Mfuko wa Elimu utakaokuwa na wajumbe wafuatao-

(a) Wajumbe wote wa Bodi ya Mfuko wa Pembejeo

(b) Wajumbe wa kamati ya uchumi, Ujenzi na Mazingira.

(c) Wawakilishi wa Tarafa zote,

(d) Mwakilishi wa Madiwani.

Majukumu ya Mkutano Mkuu.

**32.** Bila kuathiri uwezo wa Bodi, Mkutano Mkuu wa Mwaka kitakuwa ndicho chombo cha-

(a) Kupokea taarifa za Ukaguzi wa Mahesabu na utendaji wa Mfuko

za mwaka.

(b) Kuteua Wakaguzi wa Hesabu za Mfuko.

(c) Kuchagua wawakilishi wawili wa Bodi kutoka miongoni na Wadau wa Kilimo.

(d) Kuchagua Bodi ya Mfuko kwa kipindi cha miaka mitano.

(e) Kuondoa/kumfukuza Mjumbe wa Bodi kwa makosa ameyafanya kwa maoni ya walio wengi katika Mkutano Mkuu.

(f) Kuthibitisha mipango ya maendeleo iliyoandaliwa na Bodi ya Mfuko wa Pembejeo kwa kipindi kijacho.

Taarifa za mapato na matumizi.

**33.** Katibu Mtendaji atatayarisha na kuwasilisha kwenye Bodi kila miezi mitatu taarifa iliyo na-

(a) Viashiria vya utendaji na taarifa nyingine zinazohusiana na shughuli za Bodi.

(b) Kazi zinazofanyika na mafanikio yaliyopatikana.

(c) Taarifa nyingine kwa kadri Bodi itakavyoona inafaa.

Taarifa za ukaguzi wa hesabu

**34.-**(1) Katibu Mtendaji atatunza hesabu na kumbukumbu za shughuli zake na atakahikisha kuwa fedha zote zilizopokelewa zinaingizwa kwenye Akaunti na kwamba malipo yote kutoka kwenye Mfuko yanafanywa kwa usahihi baada ya kuidhinishwa na utaweka uthibiti wa kutosha wa mali zake pamoja na madeni.

(2) Hesabu za Mwaka za Mfuko wa Pembejeo za Kilimo wa

Halmashauri zitakaguliwa na Mkaguzi na Mtaalamu mwenye sifa ya ukaguzi aliyesajiliwa chini ya Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi ya Mwaka 1972 na ambaye ameteuliwa na Mkutano Mkuu.

(3) Ndani yakipindi cha miezi sita baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha Bodi itatayarisha na kuwasilisha kwa Halmashauri Taarifa ya Fedha ya mwaka huo ambayo itajumuisha-

(a) Taarifa za Fedha

(b) Viashiria vya utendaji na taarifa nyingine zinazohusina nazo.

(c) Taarifa ya utekelezaji ya Mfuko wa Elimu wa Halmashauri.

Bodi kuwa na uwezo wa kukagua

**35.** Bodi itakuwa na madaraka ya kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa hesabu za Mfuko wa Pembejeo.

Adhabu.

**36.** Mtu yeyote ambaye;

(a) Atakwenda kinyume na masharti ya Hati rasmi hii au;

(b) Atakayefanya kitendo chochote ambacho kitazuia Bodi au kamati Tendaji kufanya kazi zake kwa ufanisi ,au;

(c) Atatumia vibaya mali na rasilimali za Mfuko wa Pembejeo na kusababisha kutofikiwa kwa malengo yaliyowekwa, au

(d) Kwa uzembe atashindwa kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Hati rasmi hii.

Atakuwa ametenda kosa la jinai na akipatikana na hatia atalipa faini isiyozidi shilingi Laki tatu (300,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi

na mbili au adhabu zote mbili yaani faini na kifungo kwa pamoja.

*Lakiri ya Halmashauri*

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo imetiwa katika Sheria Ndogo hizi, katika kikao chake cha Baraza la madiwani kilichoketi leo tarehe……………mwezi,,,,,,,,,,,,,,,,,,mwaka 2014 mbele ya wafuataao:-

……………………………………………..
Judathadeus J. Mboya
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**ROMBO**.

……………………………………………
Mhe. Antony J. Tesha
**MWENYEKITI**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**ROMBO.**

Nakubali.

…………………………………………
Mhe. Mizengo P. Pinda (MB)
**WAZIRI MKUU.**

DODOMA,
30 Juni, 2014